

Mtwara Kuchehele...



Mh. Hawa Ghasia (Mb),
Waziri TAMISEMI.



Mh. Musa S. Ndazigula,
Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya Mtwara.



Iddi A. Mshili,
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara.



JARIDA LIMEANDALIWA KWA USHIRIKIANO WA



YALIYOMO

UK

TAHARIRI YA MKURUGENZI.....	3
RAMANI, DIRA NA DHIMA YA HALMASHAURI.....	4
TASAF: KAYA MASKINI MTWARA KUPATA RUZUKU.....	5
WAH. MADIWANI WAPIGA KAMBI SIKU 3 NAMTUMBUKA KUSAIDIA UJENZI WA MIUNDOMBINU.....	6
UTUMISHI NA MIPANGO WANUFAIKA NA MIFUMO YA TAARIFA KIUTENDAJI.....	7
MRADI WA MAJI MNYAWI AHUENI KWA WATUMIAJI.....	8
OFISI YA KIJJI NACHENJELE MFANO WA UTEKELEZAJI MIRADI YA MAENDELEO.....	9
PICHA NA MATUKIO.....	10
WANANCHI: "TUNAHITAJI ELIMU ZAIDI KUHUSU STAKA- BADHI GHALANI".....	11
GIZ-SULGO YAWAJENGEA UWEZO KIUTENDAJI WAJUMBE MABARAZA YA KATA.....	12
WARATIBU ELIMU WATAKIWA KUSIMAMIA MAENDELEO YA TAALUMA KIUFANISI ZAIDI.....	13
MIUNDOMBINU AFYA KUBORESHWA ZAIDI.....	14
KILIMO CHA UMWAGILIAJI BONDE LA MAHURUNGA.....	15
MMUYA: KUPITIA MICHEZO JAMII ITANUFAIKA KIELIMU NA AJIRA.....	16



"UMASKINI WA MAWAZO NI MKUBWWA KULIKO UMASKINI WOWOTE" **J. K. NYERERE**

Ni kweli ni heri mtu ukose fedha kuliko mawazo, mawazo ndo msingi wa utajiri, jamii yeyote yenye kutumia mawazo yao vizuri na kukifanyia kazi kile wanachokiwaza kiufasaha mara zote ufanikiwa katika shughuli zao.

Wanafalsafa mbalimbali wamehsawahi kuongea kwamba "...ili uweze kuendelea yakupasa kujikomboa katika utumwa wa kifikra.." Waliona mbali, kuna binadamu wanakuwa na mawazo mgando na maranyingi hawapendi kujiongeza kimawazo wala mtazamo kila kitu kwao ni kigumu wanaishia kulaumu waliowapa dhamana ya kuwaongoza, ni kweli wapo viongozi wanaokosea sana majukumu yao lakini ushawahi kujiuliza mara ngapi uliwakosoa na kuwaonesha njia mbadala ya kufanya, tuachane na hilo.

Tanzania ya sasa inakadiriwa kuwa na tabaka la vijana linalofikia zaidi ya 60% ya Watanzania wote, na wengi wao ni waathirika kama si kukosa elimu basi wana elimu ila ajira hawana, kwangu mimi ajira ni nini?...ajira ni kazi yeyote halali inayoweza ku-kuingizia kipato. Vijana wenzangu tuamke na kuchangamkia fursa zilizopo ili kukabiliwa na changamoto za maisha, kuna mambo mengi ya kufanya ili kujiongeza kipato na mwishowe kuanzisha biashara kubwa na yenye tija, lakini hivi vyote haviwezi kukamilika kama hutaweza kutumia Mawazo yako vizuri na kujenga taswira ya mradi unaothubutu kuufanya.

Kwa mfano sasa hivi kuna fursa nyingi za kuweza kuandaa mtaji wa biashara kama tu una malengo mazuri katika mawazo yako, mfano mzuri ni **"VICOBA"** (Village Community Bank) ambapo unaweza kujiunga kwa lengo la kupata mtaji, ukifanikiwa kupata mtaji unanzisha biashara ambapo hapo sasa unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo;

Kuweka akiba, kuwa na nidhamu ya fedha, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuweka kumbukumbu ya mapato na matumizi, ukizingatia hayo utafanikiwa katika wazo lako la biashara.

Hayati Mwalimu Nyerere aliona mbali kwa kusema hayo maneno. Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi, mawzo yake bado yapo hai na tunayatumia.

Kijana wa sasa husisubiri mpaka uajiriwe anza kujishughulisha kwa kile unachokiwaza kitakuletea mafanikio katika maisha yako, inabidi uanze kutengeneza ajira kwa watu na si kuisaka ajira, tuache kulalamika yatupasa kutambua maendeleo tunayo wenyewe na **"MAWAZO NI MTAJI MKUBWA KULIKO FEDHA"**

Tangaza Biashara yako kupitia Mtwara kuchelee ili upate Tija katika biashara yako, Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia S. L. P 528 Mtwara. au 023-2333928 0783 037242 (Afisa Habari) Barua pepe: mtwararural@gmail.com bilalisack19@yahoo.com Pia kwa maoni na ushauri waweza kutumia anuani zilizotajwa hapo juuu.



Ndg. Iddi A. Mshilli,
Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara

Ndugu msomaji,

Napenda kuchukua nafasi hii kujitambulisha kwako, mimi ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Vijijini, nina faraja kuiongoza halmashauri ambayo ni muhimu sana katika maendeleo ya Watu wa Mtwara na Tanzania kwa ujumla, pia napenda kuwafahamisha kwamba halmashauri imeamua kuanzisha Jarida lake litakalokuwa lina toa taarifa mbalimbali za maendeleo Kiuchumi, Kijamii, Kisiasa na changamoto nyinginezo zinazoigusa Halmashauri ya Wilaya na wakaazi wake.

Vilevile litatumika kama njia mzuri ya kupata mrejesho wa malalamiko, mapendekezo, ushauri, kukosoa na hata jinsi ya kuboresha huduma mbalimbali kwa wananchi wote, hivyo basi kwa niaba ya wataalamu wangu wote nakuomba ulipokee Jarida hili kwani ni njia kuu ya kuimarisha mahusiano yetu na wananchi kwa njia ya Mawasiliano, nina amini mawasiliano haya yatafungua kero mbalimbali za kimaasiliano kati ya Halmashauri na wananchi.

Jarida linaitwa **“MTWARA KUCHELE”** ikimaanisha Mtwara imeamka na kuchangamka hasa kiuchumi, kijamii na kisiasa hivyo inabidi kuchangamkia fursa zote zinazojitokeza katika kukidhi matakwa ya wananchi, kupitia jarida hili zita kuwa zinaonesha baadhi ya fursa na jinsi Halmashauri inavyotanzua changamoto za kuzifikia.

Kwa upande wa zao la korosho nawaomba wakulima wazidi kusimamia mashamba yao ili wazidi kunufaika wakati wa mauzo, pia nawasisitiza kuongeza zao lingine kama vile Ufuta ili liwe mbadala wa korosho kwani kwa sasa linaonesha kuwa na soko zuri.

Pia napenda kuwashauri wananchi wawatumie wataalamu wa kilimo walio katika vijiji na kata kwa ujumla ili wapate maelekezo ya kulima mazao ya Chakula na biashara kama vile ufuta, muhogo ili kujiongezea kipato na kukabiliana na ugumu wa maisha kwani Halmashauri imewaleta huko

kwaajili ya kuhudumia raia, kuhusu suala la elimu kuhusu suala la elimu

Nawaagiza wazazi na walezi kuhakikisha wanajipanga na kuwapeleka watoto wao kupata elimu kwani ndiyo mkombozi pekee katika kujikwamua na changamoto za maisha.

Napenda kuwahasa wananchi wajiunge na huduma ya (CHF) ili kuwarahisishia kupata huduma ya afya kuliko malipo ya papo kwa papo ambayo yanagharimu fedha nyingi tofauti na Tsh. 5000 unayotakiwa kulipa kwa mwaka katika mfumo huo, unachotakiwa ni kujikusanya watu watano na kufanya usajiri.


Zaidi ya hapo, naomba ujitambue kwamba wewe ndiye mdau wa kwanza wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na katika hilo yakupasa kushirikiana na wataalamu wako katika kuleta maendeleo, wale wote wenye sifa ya kulipa kodi au ushuru wowote, wafanyabiashara, unaagizwa kufanya hivyo kwa wakati kwani makusanyo hayo huwa yanarudishwa tena kwenu ili kufanikisha shughuli za kimaendeleo, hivyo ni jukumu lako kuanza kuhamasika na kuchangia pato la halmashauri.

Nawaomba muongeze mahudhurio katika vikao na mikutano mikuu ya vijiji ili kuweza kutoa ushirikiano wa kubuni miradi ya maendeleo inayoleta tija kwa walengwa kwani kwa kupitia mikutano hiyo Halmashauri inapata takwimu halisi ya wananchi wenye uhitaji katika kila kijiji na miradi mtakayoipendekeza.

Mwisho bila kuwakwaza napenda mlipokee Jarida lenu la *Mtwara kuchele* liwe linawapa habari za kina na uhakika zaidi, natanguliza shukrani za dhati na Jipatie nakala yako ya jarida ili upate taarifa za uhakika, asante sana

Ramani, Dira na Dhima ya H/W Mtwara.

MTWARA RURAL: Administrative Boundaries, Wards, Villages and Road Network




Dhamira na Dira ya Halmashauri W/Mtwara

Dhima.

“Kuandaa mazingira rafiki kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara”

DIRA

”Kuimarisha maendeleo endelevu kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ifikapo mwaka 2016”



“Mtwara Kuchelee kila baada ya miezi mitatu...Januari 2014”

TASAF: Kaya maskini Mtwara kupata ruzuku ya msingi kuendeshea maisha.

Na Isack Bilali

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara kanali mstahafu Joseph Simbakalia amewaagiza wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara kuzingatia maadili wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ameyasema hayo wakati wa uzinduzi wa mradi wa TASAF awamu ya tatu ambao umelenga kunusuru kaya masikini kwa kuzipatia Ruzuku na kuzisaidia kuanzisha na kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo wanayoishi.

Warsha ya uzinduzi wa mradi huo ilifanyika katika ukumbi wa Parish Mtwara, iliyojumuisha wataalamu mbalimbali na waheshimiwa madiwani wa Halmashauri hiyo.

Akiongezea agizo hilo mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mh. Wilman K. Ndile amewaasa wale wote watakaosimamia utekelezaji wa mradi huo ni vizuri wakazingatia uwajibikaji ili kuleta tija na ufanisi kwa walengwa

Kwa upande wake kaimu Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ndg. A. Mpenye alitanabaisha kwamba kwa upande wake ameiandaa timu ya wataalamu wapatao hamsini (50) ambao watashirikiana na wataalamu kutoka TASAF makao makuu ambao watashirikiana katika kila hatua ili kuleta matokeo yaliyo na tija, pia aliwaasa wataalamu walio-teuliwa wazingatie kile kinachowapeleka na matokeo yeyote yatakayopatikana yatakuwa yanaonesha sura ya halmashauri kwa ujumla.

Kwa upande wa Kaimu mkurugenzi wa TASAF amebainisha kuwa mradi huo upo na wameufanyia utafiti wa kina na kuna vigezo maalumu vya kuweza kumtambua maskini wa kweli hivyo ni vigumu kwa mtu ambaye si mlengwa kuingia katika mpango huo.

Pampja na hayo amewahasa wataalamu hao kuwa makini na takwimu zote watakazozikusanya kwani uhakiki utafanywa kwa makini ili kubaini kaya masikini, mradi huo umeweka wazi kiasi ambacho watasaidiwa kaya masikini kuwa ni Dola tano ya Marekani kwa kila mwezi hii ni ya msingi na dola tano nyingine itotokana na kaya husika kutimiza masharti kadhaa kama vile ikibainika kwamba kaya ni maskini na inajitahidi kuzingatia kusimamia malezi ya watoto kama vile mahudhurio ya shule na afya kwa mama na motto basi hao watapata na kufanya jumla ya dola kumi mabayo kwa sasa ni sawa na 16,000/=

Vilevile ametanabaisha kwamba kaya itakayokuwa na uwezo wa kubuni mradi na watu wa kufanya kazi basi TASAF itakuwa pamoja nao katika kuwawezesha na wengine watapata ujira ambao ni Tsh 2000 hadi 2500 kwa siku, kwa mujibu wa Mwakilishi wa Mkurugenzi wa TASAF amebainisha kwamba zoezi la ukusanyaji wa takwimu kutambua kaya masikini litafanyika kwa uangalifu kwa kushirikiana na wananchi na wataalamu ili kuleta matokeo yaliyo na tija kwani wanaamini kupitia wananchi wenyewe wanaweza kutambua na kuthibitisha kaya ambayo ni masikini kwa uhakika zaidi, hivyobasi amewaasa wananchi watoe ushirikiano wa kutoa sha ili kufanikisha zoezi husika bila kuleta udanganyifu.

Pia alitanabaisha kwamba udanganyifu wowote utakaofanyika utatambulika kwani marabaada ya kukusanya takwimu hizo kuna kipimo maalum cha kutthibitisha sifa halali cha kaya inayohitajika na kinatumia utaalumu wa kisayansi hivyo ni rahisi kutambua udanganyifu wowote.



Mgeni rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara akifungua rasmi utekelezaji wa Mradi wa TASAF awamu ya tatu, kunusuru kaya maskini.



Picha ya pamoja ya Mgeni rasmi na wataalamu 50 wa H/W Mtwara walio-teuliwa kufanya kazi na TASAF III



Picha ya pamoja ya mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali mstahafu *Joseph Simbakalia*, akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mh. *Wilman K. Ndile*, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mtwara Mh. *Musa S. Ndzigula*, Kaimu Mkurugenzi TASAF, Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara *Ali Mpenye* na waheshimiwa Madiwani, mara baada ya kufungua warsha ukumbi wa Parish Mtwara (Picha na Afisa Habari H/W Mtwara)

“SIRI YA KUFANIKISHA UJENZI WA OFISI YA UTAWALA NI KUSHIRIKIANA NA WANANCHI” - AFISA TARAFI ZIWANI



Mh. Hawa A. Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, amekua chachu ya maendeleo ya Jimbo la Mtwara Vijijini.



Mh. Diwani kata ya Ziwani akiwa na Afisa kilimo na VEO, mbele ya Jengo la Ofisi..



Maafisa wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wananchi wao.

Francis Mkuti, Afisa Tarafa Ziwani akiwa katika ufuatiliaji wa ujenzi wa jengo la ofisi ulio katika hatua za umaliziaji

Na Isack Bilali

Moja kati ya changamoto kubwa inayoisumbua Serikali ni ukosefu wa majengo ya ofisi hasa katika sekta ya Utawala kwa ngazi ya Kijiji, Kata na Tarafa kiasi kwamba baadhi ya Maafisa wanaopeleka kuhudumia wananchi vijijini wanakutana na mazingira magumu kiutendaji kutokana na ukosefu wa majengo ya utawala na mara nyingine inaweza kutumiwa nyumba ya mmoja wa wananchi kama ofisi, kitu ambacho hakileti picha mzuri hasa linapokuja suala la kumuwajibisha mtu aliyewakodisha nyumba yake.

Kwa kulitambua hilo Afisa Tarafa ya Ziwani kwa kushirikiana na watendaji wa kata, kijiji na wananchi wameamua kwa pamoja kuhakikisha wanapata Ofisi yao ili kupunguza hadha waliyokuwa wanaipata wakati wantumia kupangisha jengo la mtu binafsi, kwani maranyigine iliwapasa kukiuka misingi ya kiutendaji ili kumridhisha mmiliki wa nyumba hiyo.

Kwa mujibu wa Afisa Tarafa Ziwani Bwn. Francis T. Mkuti, ametanabaiisha kuwa ujenzi wa ofisi hiyo ambayo itatumika na Afisa Tarafa, Afisa Mtendaji wa Kata na Afisa Mtendaji wa Kijiji, ipo katika kijiji cha Nambekeketela, Kata ya Ziwani, Tarafa ya Ziwani, ujenzi wake ulianza mwaka 2009 kwa kuhamasisha watu wajitolee hivyo yeye mwenyewe akishirikiana na watendaji wake na wananchi walianza kufyatua Tofali na kuchimba msingi.

Ndipo Mh. Hawa A. Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini aliweza kuchangia kiasi cha Tsh. 2,200,000/= ili kufanikisha ujenzi huo, kitendo heho kilizidi kuwatia nguvu wananchi na uongozi wa ujumla na kuzidi kupata hamasa ya kujitolea zaidi.

Vilvile Halmashauri ya Wilaya Mtwara haikuwa nyuma katika kuwaongezea nguvu wanchi wa tarafa ya Ziwani kwani imewezakuchangia kiasi chana mchnago wa kiufundi kutoka

Kwa waandisi wa ujenzi ili kuliimarisha jingo hilo.

Mpaka jingo kuisha inakadiriwa itagharimu Tsh. 42,000,000/= na lina vyumba 8 na ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchuka watu 70, hadi sasa limefikia zaidi ya 80% ya ujenzi wake.

Kwa niaba ya uongozi na wananchi wa Ziwani Afisa tarafa anawashukuru wote waliojitoa kufanikisha ujenzi huo na Nafasi hadimu ya kutembelewa na mwenge kasha kiongozi wa mbio kufungua rasmi Jengo hilo kwani ilizidi kuwatia hamasa wananchi wa Nambekeketela.

Pamoja na hayo changamoto kubwa waliyonyo ni kwa upande wa umaliziaji (Finishing) wanahitaji Samani za ofisi, wamefanikiwa kuvuta nguzo ya umeme wenye moto tayari na nyaraka zote zimewasilishwa katika ofisi husika hivyo wanaomba kusaaidiwa kwa hatua iliyobakia ili waweze kupata huduma stahiki.

LAWSON mfumo wa taarifa za watumishi unaoleta tija.

Na Isack Bilali



Maisha Mtipa, Idara ya Utumishi

Idara ya Utumishi imebainisha kwamba kwa sasa mfumo wa kuandaa na kutuma taarifa za watumishi unaofahamika kama LAWSON umeweza kutatua changamoto nyingi za kiutendaji katika idara hiyo.

Akiongea ofisini kwake kaimu Afisa utumishi wa H/W Mtwara Ndg. Maisha Mtipa alifafanua kwamba mfumo huo umeleta ufanisi kubwa kwasababu unaweza kuhudumia watumishi wengi kwa wakati mmoja tofauti na awali.

Mfumo huu umeleta ufanisi katika kutuma taarifa za watumishi wanya makao makuu ya Utumishi, hivyo inarahisisha kuingizwa katika mshahara ndani ya mwezi mmoja mara baada ya kupata ajira.

Vilevile imejidihirisha kwamba madai ya uhamisho yanazidi kupungua siku hadi siku kwani mtumishi akishapata uhamisho na taarifa zake kuingizwa katika mfumo huu basi inakuwa rahisi sana kupata haki zake za msingi kwa wakati, kitendo hiki kinapunguza mlundikano wa barua za madi katika Idara ya Utumishi.

Juu ya hapo kaimu Afisa utumishi huyo aki-shirikiana na wenzake Bwn. Abdulatif A. Mkata na Bi. Georgina Peter, wameonesha kupendezwa kwa ufanisi wa mfumo huo kwani umeimarisha ushirikiano na ukaribu kiutendaji kati yao na makao makuu ya Utumishi.

Changamoto kubwa katika kutumia mfumo huu ni pale mtandao unaposumubua kwani bila kuwa na mtandao huwezi kufanya kitu chochote



Abdulatif A. Mkata Idara ya Utumishi.



Georgina Peter, Idara ya Utumishi.

Idara ya mipango yaainisha Ubora wa PLAN REP katika Bajeti

Idara ya mipango katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara imebainisha kuwa mfumo maalumu wa utayarishaji makadirio ya mapato na matumizi (bajeti) unarahisisha katika kuainisha bajeti ya kila idara na vitengo vyake kwa haraka sana.

Akifafanua zaidi ndg Dadi alisema kwamba mfumo huo unarahisisha kuandaa na kuchapisha vitabu vya (MTEF) vinavyochambua mipango na matumizi ya bajeti, wakati huo huo inaokoa muda wakati wa kubainisha na kupanga utekelezaji wa miradi.

Kwa mujibu wa ndg. Fundikira Mchumi kutoka idara hiyo amefafanua kwamba mfumo huo unaenda sawa na "O and OD" yani fursa na vikwazo katika maendeleo ambao unasaidi kugundua vikwazo vinyavyokinzana na fursa zilizopo katika kutafuta maendeleo.

Mfumo huu unasaidia kutambua maeneo ya kihistoria ambayo hayafai kuanzisha mradi

wowote, hali hii inatokana na mfumo wa uandaaji wa bajeti husika kuanzia katika ngazi ya kijiji ambako wanatakiwa kuibua miradi na kuiwasilisha ofisi ya mipango ambapo wanafanya uchambuzi ya miradi ilyopendekezwa kwa kuzingati vipaumbele ambavyo ni vya kitaifa kupitia sera za Serikali na Chama kinachotawala.

Zaidi ya hapo mfumo huu unatoa mwongozo wa bajeti inayofuata na jinsi inavyotakiwa kuwa.

Pia alifafanua kwamba changamoto wanazokutana nazo wakati wa kuandaa bajeti ni nyingi lakini chache kati ya hizo ni, uelewa mdogo wa watendaji katika kuandaa kuanzia ngazi ya chini hadi Halmashauri.

Utofauti wa vipaumbele halali hali inayosababisha kukosekana kwa uhalisia kati ya watekelezaji na walengwa.

Juu ya hapo imebainishwa kwamba mfumo unatoa mapendekezo kwa wakati lakini

tatizo linakuwa ucheleweshwaji wa rasilimali fedha za kuendesha miradi husika, hivo inasababisha miradi mingi kutokamilika kwa wakati.

Mkuu wa idara ya mipango ndg. Mihambwa amethibitisha Ubora wa Plan Rep na changamoto zilizoainishwa na wasaidizi wake



Afisa Mipango (W), Bwn. Shaban Millao. akiwa ofisini kwake.

Mradi wa maji Mnyawi waleta ahueni kwa watumiaji wake

• Wahudumia kata tano

Na Isack Bilali

Wananchi wa Nanyamba Wilayani Mtwara wameipongeza Serikali kupitia Halmashauri yao kwa kuzidi kuwaboresha mradi wa maji Mnyawi ambao unahudumia takribani kata tano na kuwaondolea hadha iliyokuwa inawasumbua kwa muda mrefu hapo mwanzo.

Kwa mujibu wa Mhandisi wa maji wilaya ya Mtwara, Mhandisi John Msengi Alizitaja kata hizo kuwa ni Nanyamba, Namtumbuka, Milan-gominne, Mbembaleo na Mtiniko.

Uborehsji huo umeambatana na ujenzi wa matanki matatu katika vijiji vya Nanyamba, Din-yecha na Namkuku ambayo yameshakamilika, huku jenereta zikiwa tayari na ukamilishaji wa usambazaji mabomba upo katika hatua za mwisho.

Mradi huo ni sehemu ya utekelezaji na ubore-shaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika mpango kazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara katika kuisaidia Jamii kupata huduma stahiki katika maisha yao ya kila siku hivyo zaidi ya watu elfu sabini na tatu (73,000) wanapata huduma ya maji kutoka mradi huo.

Alizidi kufafanua kuwa mradi huo ulianza mwezi Oktoba, 2012 na muendeleo wa ukarabati wake umeanza April 2013 na unategemewa kumalizika mwezi Disemba mwaka huu, utagharimu kiasi cha Tsh bilioni tatu nukta mbili (3.2 bn) hivyo aliwaasa wananchi kuwa walenzi wa miundombinu ili kuimarisha mradi huo kwa-kuwa fedha inayotumika ni sehemu ya kodi zao wenyewe.



Mhandisi wa Maji Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Mhandisi John Msengi akiwa Ofisini.

Aliongeza kuwa kwa sasa maboresho ya mradi huo yameanza kuwanufaisha watu wa Nanyamba, Milangominne na Mbembaleo huku taratibu za kuwapata wakandarasi wazuri kwaajili ya kata za Mtiniko, Mtimbwilibwi na Namtumbuka unakaribia kukamilika.

Changamoto kubwa zinazokabili mradi huo ni jinsi ya kuwapata wakandarasi walio na sifa, rasilimali fedha zinachelewa kuja na kusa-babisha mradi kutoenda kwa wakati uliopangwa na mwisho ni uharibifu wa miundombinu ya mradi, kwahiyo mhandisi wa maji alizidi kuwaasa wananchi wazidi kujenga mazingira rafiki kwa Mradi huo kwa kulinda miundombinu na vyanzo vya maji ili kuuwezesha mradi huo kuendelea kuwahudumia kwa muda mrefu.

Asilimia kubwa ya wananchi wamekuwa na uelewa hivyo wanashirikiana kwa karibu na wataalamu tangu mradi unaanza hadi sasa unapoendelea kutoa huduma kwa jamii na ni suala la kujivunia kwani mradi huo umekuwa kama mkombozi katika tatizo lililokuwa linawasumbua kwa kipindi kirefu wananchi kwa ujumla wameupokea vizuri mradi huo na wameahidi kuulinda.

Kwa upande wa wananchi wamekiri kuwa mradi huo umeweza kuwakomboa sana ukilinganisha na hapo awali ambapo walikuwa wanapata shida sana hivyo wanaiunga mkono Halmashauri.

Zaidi ya hapo Mhandisi alitanabaisha kuwa kuna miradi mingine inayoendelea kuunganishwa ili kupunguza hadha ya maji iliyopo mfano mzuri ni mradi wa maji Mpapura kwenda Liowa ambao utahudumia vijiji vitano ambavyo ni Mpapura, Nanyani, Utende, Mabatini na Liowa na utagharimu takribani Milioni mia saba na hamsini (Tsh 750,000,000).

Huduma ya maji ni sehemu ya pato la Halmashauri kwakuwa maji yanayopatikana yanuzwa kwa Tsh 50 kwa lita 10 na fedha inayopatikana inapelekwa wilayani ili kuwezesha kutumika kwenye miradi mingine na ukarabati wa miundombinu ya miradi na hata kuboresha na kulipa wafanyakazi wa mradi husika.



- 1 Tanki la maji likipakwa rangi.
- 2 Tanki linalosambaza maji kutoka kwenye chanzo kwenda kwenye matanki mengine
- 3 Genereta kubwa linalofua umeme kwaajili ya kuendesha mitambo ya maji
- 4 Mafundi wakimalizia kufunga pampu.
- 5 Mhandisi akijadiliana na mafundi wakati wa ukaguzi wa mradi.

Ofisi ya kijiji Nachenjele mfano wa utekelezaji miradi ya ujenzi kata ya Mbawala.



1

Sera ya serikali ya Jamhuri ya Tanzania inasisitiza sana wananchi kujitolea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili iweze kutoa msaada katika ukamilishaji wa mradi husika.

Hali hii inatokana na nia ya Serikali katika ku-shirikisha wananchi kuibua, kuandaa na kutekeleza miradi mbalimbali kuanzia ngazi ya kijiji/ mtaa na kuendelea, vilevile inasaidia kuweka wazi gharama za mradi kwa wananchi na maranyingine mradi ukishakamilika inakuwa ni rahisi kuwajibika katika suala zima la kuulinda na kuundesha kwa tija zaidi.

Kutokana na sera hii wananchi wa Kijiji cha Nachenjele kata ya Mbawala kupitia hamasa za viongozi wao wa kijiji, kata na Wilaya waliamua kuunga mkono Sera ya kujitolea na kuhamishia nguvu zao zote katika ujenzi wa Ofisi ya Kijiji.

Kwa mujibu wa Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Nachenjele ndg. Saidi Mwindi amesema kwamba ujenzi huo uliridhiwa katika kikao cha serikali ya kijiji, wakachaguliwa m/kiti na katibu wa ujenzi

ambao ni Zainabu I. Chikota (M/kiti) na Daudi M. Manjavila (katibu).

Mara baada ya kuchaguliwa kazi kubwa waliyokuwa nayo ilikuwa ni kuanza kuhamasisha jamii ili wafahamu umuhimu wa kujitolea katika utekelezaji wa mradi huo, ndipo mnamo mwaka 2009 ujenzi ukaanza kwa kuandaa na kusafisha kiwanja kwa kutumia nguvukazi kutoka kwa raia wenyewe.

Rasilimali fedha iliyotumika imetokana na mchanganuo ufuatao Ruzuku kutoka Serikalini ni 3,584,000/=, Mh. Mbunge 1,500,000/=, Wananchi 1,720,000/= na S/ Kijiji kupitia mapato ya ndani 899,000/= na kufanya jumla kuu kuwa Tsh 7,703,000/=.

Mpaka sasa jengo limekamilika lina vyumba vitano ukumbi wa mikutano, mahabusu kila chumba kina maelezo juu ya mlango.



2



3



Mh. Ali Faki Nalinga, Diwani wa Kata ya Mbawala akiwa katika vazi rasmi tayari kwa kikao cha Baraza la Madiwani.



4

Kituo cha Mbawala juu chapata mshindi wa ligi daraja la nne

Klabu ya soka ya New Star Mbawala juu, imefanikiwa kukamata usukuni wa mashindano ya ligi daraja la nne katika kituo cha Mbawala, kituo hicho kilichokuwa na timu 6 kimefanikiwa kumaliza michezo yake kwa wakati, na kumtoa mshindi New Star (alama 10) akifuatiwa na Mpinzani wake wa jadi Chimbuko F.C (alama 7), timu zote zitaungana kushiriki hatua inayofuata ambayo itakutanisha washindi kutoka vituo vingine.



MAELEZO YA PICHA:

1. JENGO LA OFISI YA KIJILI NACHENJELE.
2. WANANCHI WAKICHEZA BAO, INAAMINIKA HAPO NDIPO WAZO LA KUJENGA OFISI LILIPOBUNIWA.
3. MTENDAJI NA MWENYEKITI WAKIWA OFISINI
4. MUONEKANO WA NDANI YA OFISI



Wanachi wakiupokea mwenge wa uhuru.



Ofisi ya Tarafa ya Ziwani mara baada ya kufunguliwa.

Sehemu ya umati wa wananchi wa kijiji cha Nambereketela wakisikiliza hotuba ya kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru alipokuwa anafungua na kuweka jiwe la msingi jengo la Utawala Tarafa ya Ziwani lenye vyumba 8.

RUSHWA NI ADUI WA HAKI, husipokee wala kutoa RUSHWA...!

UJENZI WA OFISI YA KATA MUUNGANO WAENDELEA ILI KUBORESHA HUDUMA KWA WANANCHI



OFISI YA KATA MUUNGANO.



JENGO JIPYA LA OFISI YA KATA MUUNGANO LIKIWA KATIKA .HATUA NZURI YA UJENZI, LINA VYUMBA 6 NA UKUMBI.

Wananchi: “Tunahitaji elimu zaidi kuhusu Stakabadhi ghalani”

Kutokana na matatizo na changamoto zilizoikumba zao la korosho serikali kupitia wizara ya kilimo iliamua kuanzisha mfumo mzuri wa kuwawezesha wakulima wa zao la korosho kuondokana na adha ya kukosa soko la uhakika kwa zao lao pindi msimu unapowadia.

Zao la korosho ni maarufu sana katika mkoa wa Mtwara na wananchi wake wanalitegemea sana kwani ndilo zao la biashara linalowawezesha kutekeleza mipango yao mbalimbali, hivyo linabakia kuwa ni uti wa mgongo wa wananchi wa kusini hususani Lindi na Mtwara.

Wakati serikali wanaamua kuanzisha mfumo huu wa stakabadhi ghalani waliamini itakuwa suluhisho la matatizo yanayolisumbua soko kwa zao la korosho, kinadharia na maelekezo yake mfumo mzima wa Stakabadhi ghalani unaonesha tija kwa mkulima, lakini kinyume na matarajio ya wengi wakulima wamegeuka na kuanza kuukosa na wengine wanafikia hatua ya kuukataa kabisa mfumo wenyewe.

Mara kadhaa imebainika kuwa kipindi cha msimu wa korosho kuna Vyama vya msingi vinamaliza kuuza korosho za na kuwalipa wakulima ela yao kwa awamu mbili bila matatizo, pia kuna vyama vingine vimeshindwa kabisa kusanifu utendaji wao na kusababisha malipo kwa Mkulima kuwa kitendawili.

Kutokana na ushahidi huo hapo juu, tatizo kubwa linaloikumba zao la korosho ni Udhaifu wa baadhi ya viongozi wenye dhamana ya kuongoza vyama husika, kwanini masema hivyo, ni kwasababu mfumo kama ulivyo haujaonesha kushindwa ila wenye dhamana ya kutumia huo mfumo ndio wenye matatizo na ndiyo sababu kuna vyama vingine vinamaliza msimu wa mavuno kwa amani na vingine lazima kipate matatizo.

“Haja ya mja unenwa, uungwana ni vitendo” katika hili ni wazi kabisa mfumo unashadidia kumsaidia Mkulima kwa asilimia zote kwa kumuhakikishia kupata thamani ya bei elekezi katika mauzo ya Korosho zake, lakini kuna “wajanja hewa” wachache wanavuruga na kusingizia mfumo, La hash! Hata kama hujui kusoma na picha nayo huioni? Ebu jilulize mfumo huo huo iweje Chama “A” kiweze kuwalipa vizuri wananchi wake, wakati huo huo Chama “B” kimeshindwa kulipa wananchi wake, sihitaji jibu, nalijua!

Kwa upande wangu naamini Elimu ya mara kwa mara kwa wananchi na viongozi wa vyama vya msingi inahitajika ili kuwaweka wazi kuhusu mfumo mzima wa stakabadhi ghalani, nasisitiza hili kwasababu kuna baadhi ya wananchi ambao hawajui kabisa maana halisi na umihimu wa Mfumo huo na wengi wao wanapatikana vijiji vya ndani kabisa, na hili ndilo

kundi kubwa ambalo linahitaji msaada wa elimu taarifa kuhusu mfumo huu, watu hawa ni wepesi kuelimishwa lakini ni wepesi zaidi kulaghaiwa na watu wenye kutumia udhaifu wa binadamu mwenzake ili kupata manufaa binafsi.

Kwahiyi aina hiyo ya watu wakishapatiwa elimu taarifa ya mfumo wa mauzo na faida zake wataweza kuleta tija katika soko la Korosho kuliko hivi sasa ambapo wameshajaziwa



fikra hasi katika uelewa wao na ndo maana wengi wao wanaamua kuuza kienyeji korosho zao kwa mtindo maarufu wa “Kangomba” na hata kushiriki kuwasaidia walanguzi wa zao hilo kutorosha mzigo bila wao kutambaua madhara ya kile wanachokifanya.

Mara nyingi wanaamua kufanya hivyo kwa kuwa uelewa wao ni mdogo na kumbuka wameshajazwa fikra hasi kuhusu Stakabadhi ghalani kwahiyi wanakuwa waathirika wanaotafuta Mkombozi na kwa wakati huo mkombozi pekee wanaehisi atawasaidia ndo huyo anaewalangua kwa kununua korosho zao kwa bei ya chini tofauti na ile elekezi na kwa kuwa analipwa fedha zote kwa wakati mmoja ambazo zinaweza kumsaidia kutatua shida chache anaamini kile anachokifanya ni bora kuliko kusubiria changamoto za Stakabadhi ghalani, Hali hii inapunguza sana pato kwaHal-mashauri.

Ninaamini watu hawa wakipewa elimu taarifa ya mara kwa mara muda mchache kabla ya msimu, kipindi msimu unaendelea na mara baada ya msimu, basi watatoa ushirikiano wa kutosha na pato linalotokana na zao la korosho litaongezeka.

Ukifanikiwa kuongea na wanachama mbalimbali wa vyama vya msingi (wakulima) tatizo kubwa

watakalo kueleza ni Kukosa taarifa sahihi na kwa wakati, vile-vile wanakosa mikutano kisheria hivyo wankuwa hawelewi kinachoendelea hali inyawafanya wahisi viongozi wao wanawaibia na ndio mana maranyingi wanafanya vurugu, si kwa kupenda ila wanafanya hivyo kama shinikizo ili wapate kile wana-chokikosa ambacho kimsingi ni haki yao kukupata.

Baada ya kupata maelezo hayo kutoka kwa wanachama wa

Chama “A”, “B” na “C” nika-jiridhisha kwamba tatizo la migogoro na vurugu kipindi cha msimu wa korosho ni kutokana na wanachama kukosa Elimu Taarifa iliyo sahihi na kwa wakati, nikaenda mbali zaidi kusadifisha ukweli wa hili, nikatembelea Chama kingine ambacho msimu uliopita na huu unaoishia hakijapatwa na migogoro nilivyojaribu kuwahoji ni njia zipi wametumia wakaniambia wana ushirikiano mzuri kati ya wakulima, serikali hivyo taarifa ya kila hatua inafika kwa wananchi kwa wakati na hata kipindi cha soko kuwa gumu huwa wanawaambia wananchi na wanawasikiliza.

Vyama vya msingi mnaombwa kushirikiana na Ofisi ya Ushirika na kutoa Elimu Taarifa kwa wanachama wenu.



Na Isack Bilali

GIZ-SULGO kuwajengea uwezo mabaraza ya kata

Shirika la maendeleo la Ujerumani lilinaloshirikiana na Serikali ya Tanzania katika serikali za mitaa GIZ-SULGO limeandaa Mafunzo (Semina) ya siku 5 kwa wajumbe wa mabaraza ya usuluhishi ya kata katika Halmashauri ya wilaya ya Mtwara, kuanzia tarehe 3-7, Desemba mwaka huu.

Mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo wajumbe wa mabaraza ya kata ili kuleta ufanisi katika utendaji wao hasa suala zima la kutoa maamuzi ya malalamiko mbalimbali yanayofikishwa mbele yao na wananchi wanaowahudumia ndani ya kata zao.

Pia kwa upande wa muaandaaji wa mafunzo hayo kutoka Shirika la maendeleo la Ujerumani Bwn. Norbet Feige alisema kwamba wamehasika kuandaa mafunzo hayo kwa kuwa wanatambua mazingira magumu wanayofanyia kazi, ukosefu wa fedha na vitendea kazi walio nao na hata kutokuwa na ofisi maalumu kwaajili ya kazi zao, hivyo basi wameamua kuwapa uwezo wa kujitambua kiutendaji kwakuwa hayo mengineyo wanaamini wataendelea kuyapata kutoka kwa serikali kadri watakavyokuwa wanapata uwezo wa kuwawezesha.

Mwezeshaji mkuu kwa upande wa hal-

mashauri ambaye ni mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara wakili Oscar Ng'itu, aliwasisitiza wajumbe hao kuwa mpaka ikifika mwisho wa mafunzo atakayowapa watakuwa na uwezo wa kufahamu umuhimu wa mipaka yao katika kupokea na kushughulikia malalamiko mbalimbali kwani huo ni msingi mmoja wapo kisheria katika kuanza mashauri lazima kufahamu makazi halali ya mlalamikaji na mlalamikiwa ili kupata uhalali wa kuanza majadiliano halali kisheria.

Pia aliwaasa kutopokea malalamiko kwa watu kwa sababu ya ukaribu walio nao kwa minajili ya kutoa maamuzi ya upendeleo hata kama mlalamikaji si mkazi wa kata husika kwani kufanya hivyo ni kinyume na sheria ambazo wanatakiwa kuzisimamia na mara nyingine ikibainika ni rahisi kwao kushtakiwa na TAKUKURU.

Juu ya hapo alitanabaisha kuwa ni kinyume na sheria kutoa maamuzi kwa upendeleo kupitia misingi ya mtu kuwa wa imani moja au kabila moja na wewe mwenye dhamana ya kutoa hayo maamuzi au kumlazimisha mwananchi ahudhuri mashauri akiwa amevaa vazi la dini Fulani kwa masharti kwamba akifanya kinyume basi shauri lake litawekwa pembeni.

Kikubwa alichowashauri wajumbe hao ni kwamba kupitia mafunzo hayo wanatakiwa wafanye majadiliano ya kina na kubadilishana uzoefu kati ya kata moja na nyingine ili wafahamu jinsi gani wanatoza faini kama gharama za baadhi ya huduma au hukumu kwa makosa yanayofanana ili mwishowe wapate ainamoja ya adhabu ambayo itakuwa

inatumika kwa kata zote za Mtwara Vijijini.

Kwa upande wa wajumbe wameyapokea vizuri mafunzo hayo na wanaamini baada ya kumaliza hizo siku tano watakuwa wameongeza ujuzi kiutendaji hivyobasi wataenda kueta mabadiliko katika utendaji wao wakizingatia yale waliyopewa na Mwezeshaji.



Picha juu Oscar Ng'itu, Mwanasheria wa Halmashauri akiwafundisha wajumbe wa Mabaraza ya kata.

Picha ya chini ni sehemu ya wajumbe wakimsikiliza mjumbe mwenzao akitoa mchango wakati wa mafunzo hayo.

Mduwi wafyatua tofali kwaajili ya ujenzi wa darasa lingine



Kamera ya Afisa habari iliwanasa wananchi wa kijiji cha Mduwi wakiwa na Mtendaji wao wa kijiji wakiendelea na kazi ya kufyatua tofali ili kujengea darasa kwa kujitolea, wote kwa pamoja walidai wameamua kufanya hivyo ili kujenga mazingira mazuri kwa kizazi kijacho na kuunga mkono sera ya serikali ya kujitolea ili serikali nayo izeze kuwasaidia na wamefanikiwa kufanya hivyo kwa kujenga darasa moja ambalo lishaanza kutumika na watoto wao.

DEO H/W Mtwara awagiza Waratibu Elimu kusimamia vizuri majukumu yao

Na Isack Bilali



Kulia ni Kaimu Afisa elimu Said Farhani akiongea na Waratibu, katikati ni aliyekuwa M/kiti Kanandamule.

Changamoto kubwa iliyotanabaishwa mbele ya mgeni rasmi ni kwamba kuna uwiano husioridhisha wa idadi ya walimu na wanafunzikutoka shule moja hadi nyingine kwa mfano kuna baadhi ya shule utakuta zina idadi ndogo ya wanafunzi lakini walimu ni wengi kiasi kwamba somo moja utakuta linafundishwa na walimu mpaka watatu na kuendelea tofauti na shule nyingine.

Juu ya hapo imebainika kwamba kuna udanganyifu mkubwa unaofanywa na walimu hasa katika kutoa visingizio kama vile vya ugonjwa na kutishiwa maisha ili apate uhamisho, tatizo ili linawahisishia kujaziwa nyaraka za ruhusa kwa haraka.

Vilevile waratibu wamelalamika kwamba ushirikiano umekuwa hafifu kutoka kwa watumishi wanaowasimamia na mara nyingine wanakuwa kama hawatambuliki mbele zao kiasi kwamba ime-wahi kutokea mtumishi kaanza kazi bila mratibu wake kufahamu uwepo wake.

Wamebainisha kuwa hizo ni baadhi ya changamoto zinazo sababisha utendaji wao kuwa unazorota kwani wakizidi kuwafuatilia wanakingiwa kifua badala ya kuwajibishwa, hivyo walimuomba mgeni rasmi ayazinagtie hayo ili wafanye kazi kwa tija zaidi.

Kwa upande wa mgeni rasmi alikiri kuwepo kwa changamoto hizo na kuahidi kuanza kuzifanyia kazi mara moja.

Mara baada ya changamoto hizo Afisa mtakwimu na vielelezo aliwataka waratibu kuwasilisha taarifa zao kwa wakati na kuwahimiza walimu wakuu

wawasilishe taarifa za mwezi kwa muda sahihi kama walivyopanga ili ziwasilishwe kwa Afisa Elimu Mkoa.

Mwisho kabisa ulifanyika uchuguzi ili kupata safu mpya ya viongozi watakaongoza kwa muda wa miaka mitatu, ambapo nafasi ya Mwenyekiti alipata Mwlm, Mohamedi Kazumari na makamu ni Salum M.Mbilinga, Katibu ni Selemani Sankwa na mweka hazina ni Mwlm Mariamu Mhina.

Akizungumza mara baada ya kukalia kiti m/kiti aliwaagiza waratibu wenzake kwenda kusimamia maazimio waliyoyapitisha hasa kusimamia ukuaji wa elimu, kukuza ushirikiano kiutendaji na kuzingatia sheria na taratibu zilizopo ili kuleta tija kazini.



Waratibu wakimsikiliza K/Afisa elimu.

Kaimu Afisa elimu Wilaya Said Farhani amewaagiza Waratibu wa elimu kata wa Halmashauri ya wilaya ya Mtwara kusimamia wajibu katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuinua kiwango cha ufanisi kielimu, ameyasema hayo wakati wa kikao kilichowakutanisha Waratibu wote wa Halmashauri kilichofanyika katika ukumbi wa ofisi ya chama cha walimu ili kujadili usimamizi wa elimu wilayani Mtwara na changamoto wana-zokutana nazo.

Sanjari na hilo Kaimu Afisa Elimu aliwapongeza waratibu hao kwa jitihada wanazozifanya kwani matunda yake yameanza kujiongesha kwa upande wa matokeo ya Darasa la saba kwani shule ya kwanza kimkoa imetoka katika Wilaya hii ambayo ni Shule ya msingi Mkubulu na imeshika nafasi ya 286 kitaifa kati ya shule zaidi ya 15,500 hivyo aliwaasa waongeze bidii ili kupata matokeo yaliyo bora zaidi.



M/kiti wa sasa wa Waratibu elimu Mohamedi Kazumari akitoa nasaha.

Mwlm akiwa na wanafunzi/mwananchi akichangia mada



MIUNDOMBINU YA AFYA KUBORESHWA ILI KUSANIFU HUDUMA



Imeaminika na kuthibitika kuwa jamii yeyote Duniani iliyopiga hatua kimaendeleo lazima wananchi wake watakuwa walishaimarika kiafya tangu awali, kwangu mimi afya ndo kila kitu kwani mtu akiwa na uimara wa afya yake hata uzalishaji unaongezeka tena kwa ufanisi mkubwa.

Kwa kuona hilo Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara inaendelea kuboresha miundombinu katika sekta ya afya Vijijini ikiwa ni sehemu ya mipango yake ya kuhakikisha huduma hiyo muhimu inapatikana kwa urahisi.

Uboreshaji huo unaambatana na utekelezaji wa miradi mbalimbali inayochagiza utoaji wa huduma ya afya kwa wananchi wa rika na makundi tofauti kulingana na mahitaji yao mfano akina mama wajawazito na watoto hawa wamepewa kipaumbele kulingana na sera ya Serikali pia kuna uchangiaji kupitia mfuko wa bima ya afya kwa jamii (CHF) ambapo mkuu wa kaya anaungana na wategemezi wake watanao na kulipia Tsh 5000/= ambapo watapata huduma katika kituo chochote cha afya kwa muda wa mwaka mzima.

Afya ya mama na motto imezingatiwa sana ili kupunguza vifo vinavyotokana na matatizo ya uzazi, hivyo wajawazito na akina mama wanaolea kwa asilimia kubwa wameweza kubadilika na wanahudhuria zahanati na kujifungulia katika vituo vya afya hali ambayo imeweza kupunguza vifo kwa kiasi kikubwa sana.

Mpango huo wa kuratibu na kuboresha afya ya mama na mtoto ni sehemu ya utekelezaji wa Malengo ya maendeleo ya Milenia kuhusu afya, ambapo yanalenga kutokomeza vifo vya mama na mtoto wakati wa uzazi.

Pia Halmashauri ina mpango wa kuhakikisha kila kijiji kilichopo ndani ya wilaya hii kina-kuwa na Zahanati yake ili kurahisisha upatikanaji wa huduma ya afya kwa jamii na hata kupuguza umbali wa kufuata huduma hiyo.

Ingawa mahitaji ni mengi sana katika huduma ya jamii, halmashauri imejitahidi kuhamasisha wananchi kuchangia ujenzi wa zahanati katika maeneo yao ili wakifikia hatua nzuri kama ya linta au gebo ndipo waweze kuongezewa nguvu kutoka serikalini na kwa kufanya hivyo sehemu nyingi wameshaanza taratibu za ujenzi wakitumia ramani kutoka kwa mhandisi wa ujenzi wilaya ili ziwe na muonekano wa aina moja.

Kwa upande wa wataalamu wa afya waganga na wauguzi Serikali inazidi kuajiri wataalamu hao na kwa sasa wanaongozwa na mganga mkuu wa Wilaya Mohamedi Mang'una, ambapo kwa upande wake ameweza kutanabai- sha kuwa kituo cha afya cha Nanguruwe kinazidi kuboreshwa ikwa kuwa na wataalamu na miundombinu yake kama vile

vifaa na majengo ya vyumba vya kulaza wagojwa ili kiweze kukidhi hadhi na kuwa hospitali ya wilaya mabadiliko haya yatakuwa yanafanya kila mara kulingana na upatikanaji wa fedha.

Juu ya hapo Halmashauri imezidi kujenga mazingira rafiki kwa wataalamu wa afya ili waweze kupatikana kwa wakati wote, hivyo basi ina hakikisha kila kwenye mpango wa kujengwa Zahanati lazima iwepo na nyumba ya mganga na muuguzi zenye uimara na za kisasa kwa gharama nafuu.



Mkuu wa Wialya ya Mtwara Mh. Wilman K. Ndile akiwa na Mganga mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mohamedi Mang'una walipotembelea kijiji cha Arusha chini kuongea na wananchi juu ya maendeleo ya ujenzi wa Zahanati.

Maelezo ya Picha:

1. Jengo la Zahanati ya Dinyecha.
2. Jengo lililoanza kujengwa na wananchi wa Kijiji cha rusha chini kwaajili ya Zahanati, Halmashauri imejipanga kuwasaidia wananchi wenye mtazamo kama huu.
3. Nyumba mbili za watumishi wa afya Mganga na muuguzi zikiwa zimemalizika.



Mpango shirikishi kati ya mwekezaji na wakulima kuongeza mavuno ya mpunga Mahurunga.



M/kiti wa Kijiji cha Kitunguli, **Musa Mnova**, akiwa na wageni ofisini kwake

Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara kupitia idara ya Kilimo imewahakikishia wananchi wa Kata ya Mahurunga wilayani humo kuwa wakiendelea kumpa ushirikiano mwekezaji wa zao la mpunga na kufanya nae kazi kwa mshikamano watapata mavuno makubwa sana.

Mwekezaji huyo ambaye ni Mtanzania amekiri kukutana na vikwazo vingi kutoka kwa wananchi wakati anakuja kutangaza nia yake uya kuwekeza lakini anaishukuru Halmashauri kwani ilisimama kidetekuaweka sawa wale waliokuwa wantia uguu kwa kuwalesha kuwa manufaa makubwa watayapata wananchi wenyewe kwani nia ya mwekezaji ni kuinua kipato chao na si kuwanyonya.

Wananchi walikubali kuingia ubia na mwekezaji huyo kwa minajili kwamba mwekezaji atakuwa anaandaa shamba lote kwa gharama zake ambapo maechukua eneo lenye ukubwa wa ekari 10000, amablo ameingia makubaliano na wakulima kuwa asilimia sitini(60%) itakuwa ya kwake na arobaaini (40%) atapata mkulima, ardhi inabakia kuwa mali ya mkulima mwenyewe.

Akiongea kwa niaba ya wananchi wake Mwenyekiti wa kijiji cha Kitunguri mahali lilipo shamba amesema kwamba wananchi wake wameanza kuelewa matakwa ya mwekezaji huyo kwa kuwa alifanya bidii kwa kuwachukua baadhi ya raia na kuwapeleka katika Wilaya ya Mbalari ili kuwaonesha mradi kama huo anaouendeleza na jinsi wananchi wa huko wanavyonufaika na aina hiyo ya uwekezaji, mara baada ya kurudi huko waliweza kuwaelimisha wenzao kuhusiana na yale waliyoyashuhudia na kwa pamoja wakaa-mua kupokea mabadilko na kumpa

ushirikiano wakitegemea kupngeza tija katika mavuno yao, pia walikfurahishwa sana kwa kupata safari iliyowapa mwanga kimtazamo.

Juu ya hapo mwanachi ambaye alishiriki katika safari hiyo alikiri kwamba ilikuwa vigumu kuamini tulichoambiwa na mwekezaji huyo hapo awali lakini mara baada ya kupelekwa Mbalari walijionea jinsi mambo yanavyokwenda, na yeye kama kijana amekuwa mstari wa mbele hata kuwashawishi wenzake kumuunga mkono Mwekezaji huyo ili wanufaika a uwepo wake, hivyo wameahidi kujenga mazingira ya ulinzi kwa mwekezaji na aniomba Serikali wazidi kumuunga mkono kwa lolote.

Mradi huo mkubwa wa kilimo cha mpunga katika bonde la mahurunga utaendeshwa kwa kutumia mitambo maalum ya umwagiliaji kwa njia ya matone ambapo maji yake yatafunwa kutoka mto Ruvuma, ivyo basi kuwa na uhakika wa kupata maji kwa kipindi muafaka, hadi hivi sasa shamba hilo lipo katika hatua ya mzuri kwani limeshapandwa na baadhi ya mimea imeshaanza kuonekana, inakidiriwa itagharimu zaid ya shilingi milioni mia tatu (Tsh 300,000,000/=) kuendesha mradi huo.

Wataalamu wa kilimo wamewasisitizia wanachi kutoa ushirikiano ili kuondokana na uvunaji wa hali ya chini na waweze kujiongezea kiwango ambapo wanaweza kuongeza kipato kwa kuuza sehemu ya mavuno yao na mengine kujiweekeka akiba, kwani kwa mujibu wa mipango ya mwekezaji ameahidi kama hali itakwenda ilivyopangwa basi ataanzisha mashine ya kukoboa ili aweze kuandaa mchele na kuingiza sokoni kitendo kitakachozalisha ajira kwa watu wa hapo, vilevile soko la zao hilo litaimarika

na mwishowe mwananchi hatategemea tena korosho peke yake.

Pamoja na hayo Halmashauri inategemea kuongeza pato lake kupitia gharama za uendeshaji na mazao yatakayopatikana yatakuwa yanaingiza faida katika ushuru wa mazao.




Mashine maalumu inayotumika kupandia mpunga.



Kifaa maalum kwaajili ya kumwagilia mpunga mali ya mwekezaji.



Muonekano wa shamba baada ya kupanda mbegu ya mpunga



Mtwara kuchele..

Michezo na Burudani



MMUYA: KUPITIA MICHEZO JAMII ITANUFAIKA KIELIMU NA AJIRA

Afisa Michezo Wilaya Bwn. Mmuya amewataka wazazi na wananchi wa Mtwara kwa ujumla kuwapa ushirikiano Vijana wao mara wanapojiingiza kwenye suala zima la Michezo kwani ni njia moja wapo ya kuhamasisha matokeo mazuri kwa kijana anayesoma na vilevile ni sehemu ya kumuongezea kipato kwa wale wasio na ajira ya moja kwa moja. Ameyasema hayo akiwa ofisini kwake wakati akiongea na mwandishi wa habari hizi, pia alifafanua kuwa mwanafunzi anapokuwa darasani anatakiwa mwili wake upate uchangamfu ili kuweza kunyambua uelewa wa kile anachofundishwa na mwalimu wake na hakuna kitu kingine kinachoweza kumfanya awe mchangamfu zaidi ya kujihusisha na michezo hivyo basi kupitia kitengo cha michezo Halmashauri imejipanga kuan-da mpango maalum wa kushirikisha michezo mashuleni ili kuinua Taaluma. Kwa upande wa ajira amesisitiza kwamba michezo kwa sasa ni sehemu ya kujipatia ajira na kuweza kuendeshea maisha, mfano mzuri ni mpira wa miguu, sanaa ya muziki, uchoraji na mengineyo, ambapo imeshadhihirika vijana wengi wanaendesha maisha yao kwa kupitia tasnia zilizotajwa hapo juu, na hii inasaidia kupunguza tatizo sugu la ajira linaloikumba Nchi yetu kinachotakiwa ni jamii na mtu mwenyewe kujipanga na kujua anachokifanya.


Akizungumzia kwa upande wa wadau wanaotakiwa kuiendeleza michezo Afisa michezo amewaomba wadau wajitokeze katika kuisimamia na kufadhili mashindano mbalimbali kama vile ligi za mpira wa miguu daraja la nne na la tatu ambazo zinaendelea hivi sasa. Kwa upande wake amebainisha kwamba alishazunguka na kuongea na viongozi wa vilabu vya mpira wa miguu katika kata 28 za Halmashauri kikubwa alichokifanya ni kuhamasisha wasajili vilabu vya kitendo ambacho kimefanyika kwa asilimia kubwa pia aliwashawishi wajiunge na ligi daraja la nne inayoendelea kitendo ambacho kimeungwa mkono, na utaratibu huo wote wa kukutana na Viongozi na uendeshaji wa ligi hizo umewezeshwa kwa ufadhili wa Mh. **Hawa A. Ghasia** (Mb) Waziri wa **TAMISEMI**. Kwa upande wake Mh. Mbunge alitoa zawadi ya mpira kwa Vilabu vilivyoweza kusajili na kuweza kufadhili uendeshaji wa ligi daraja la nne inayoendelea katika vituo mbalimbali ndani ya Mtwara vijijini, pamoja na kutoa burudani lakini pia imeonesha michezo inaleta na kuimarisha mshikamano na urafiki baina ya wananchi. Juu ya hapo kitengo cha michezo kilifanikiwa kumpeleka mshiriki wa Mbio ndefu za Riadha Mwalimu **Juma M. Libanda** huko Dar es salaam kushiriki Mbio za Uhuru, ingawa ilikuwa ni mara yake ya



Kwanza kushiriki katika mahsindano kama hayo kijana huyo aliweza kuwa mshiriki wa 11 kati ya 40 waliokimbia mbio hizo kwahiyo aliweza kujijengea hali ya kujiamini kitendo ambacho kimempa hamasa ya kujikita katika mchezo huo ambapo kwa sasa anajichua kwa umakini zaidi ili aweze kushiriki mashindano mengine yatakayo jitokeza kama vile “Kilimanjaro Marathon”. Wadau mnaombwa kumuunga mkono kijana kama huyu ambaye amejitoa kiujasiri kupeperusha sifa ya WanaMtwara, maranyingi anakimbia alfajiri kwa km 30 baada ya hapo anajiandaa na kwenda kazini kufundisha katika Shule ya Sekondari Ndumbwe, ratiba kwake haimsumbui kwani amejipangalia mfumo mzuri ambao haungiliani kimajukumu.



2



3



4

(1.) Mh. **Hawa A. Ghasia**, (Mb), Waziri wa **TAMISEMI**.

(2.) **Nicholaus Mmuya**, Afisa Michezo Wilaya akiwa ofisini.

(3) **Mwlm. Juma Libanda**, Mshiriki wa mbio ndefu za Uhuru kutoka H/W Mtwara.

(4) New Star Mbwala